# LEARNING BY EAR 2012

## "Wasaliti walo karibu – Hadithi inayoangazia dhulma zinazoambatana na ngono"

## EPISODE 1: "Waso na hatia"

**AUTHOR: Chrispin Mwakideu**
**EDITOR: Andrea Schmidt, Pendo Paul**
**Proofreader: Pendo Paul**

**List of characters by scene:**

**SCENE ONE: PATO AND SEREFA AT MR. MANENO'S OFFICE**

- **Pato (f, 16)**
- **Serefa (f, 40)**
- **Mr. Maneno (m, 45)**
- **Narrator (m/f, around 30)**

**SCENE TWO: NURU AND JENA AT A DISTANT WATERHOLE**

- **Nuru (f, 30)**
- **Jena (f, 25)**
- **Narrator (m/f, around 30)**

**SCENE THREE: ALLAN, PRECIOUS AND JOE IN CAFETERIA**

- **Allan (m, 10)**
- **Precious (f, 30)**
- **Joe (m, 45)**

- **Narrator (m/f, around 30)**

**SCENE FOUR: NURU AT THE WATERHOLE**

- **Nuru (f, 30)**
- **4-5 rebels (m, 15-50)**
- **Narrator (m/f, around 30)**

**UTANGULIZI:**

Habari na karibu tena katika kipindi hiki cha **Noa bongo, Jenga maisha yako**. Ungana nasi katika hadithi hii mpya itakayosimuliwa katika vipindi kumi vijavyo inayojulikana kama, **"Wasaliti walo karibu".** Hadithi hii inahusu suala nyeti linaloathiri kila nchi duniani: Dhulma za ngono. Dhulma za ngono humaanisha kitendo chochote kinachohusika na ngono pasipo azma, hiyari, au makubaliano kati ya wawili. Kama tutakavyosikia katika makala haya, mambo haya hayatokei mahala palipo na machafuko ya amani pekee; hasha! Hutokea popote. Tutakutana na wahusika watatu wanaoishi katika nchi ya Baruti: Pato, binti wa miaka 16 anayesoma katika shule ya mseto, Allan, kijana wa miaka 10 anayeishi na ami yake, Joe, na mwisho Nuru, mwanamke anayeishi karibu na kichaka kilichoficha magaidi. Wote watajikuta kwa njia moja au nyengine wakiwa wamedhulumiwa kingono, na watajaribu kuishi na hali hii ngumu inayowasibu. Kisha, iwavyo, pia tutakutana na Judy, anayefanya kazi na shirika la ' Kupinga dhulma za ngono". Kipindi hiki cha kwanza kinaitwa **'Waso na hatia'.** Tunaanza hadithi yetu na Pato, mwanagenzi anayetaka kuanza masomo shule ya mseto. Mamake, Serefa amemleta katika ofisi ya mwalimu mkuu, Bw. Maneno.

**SCENE ONE: PATO NA MAMAKE AFISINI KWA BW. MANENO**

1. **MANENO:** Karibuni shule ya upili ya Kilindi! Jina lako ni Pato Serefa, sivyo?

2. **PATO:** Naam Mwalimu, naitwa Pato Serefa.

3. **MANENO:** Tafadhali hebu fungua sanduku lako? Nataka kuona umebeba nini ndani.

4. **SEREFA:** **(shocked)** Ati?! Samahani Bw....

5. **MANENO:** **(calmly)** Maneno.

6. **SEREFA:** Bw. Maneno sidhani kama hivyo ni sawa. Binti yangu huyu ana miaka kumi na sita sasa. Kwani haruhusiwi kuwa na nafasi yake ya usiri? Anafaa kuwa na mambo yake ya kibinafsi, karibuni atakua mtu mzima!

7. **MANENO:** Mama, sianzi leo kutazama wabebacho wanafunzi. Muhimu ni kusadikisha kuwa habebi vitu vilivyo haramishwa na shule. Huu ni utaratibu wa shule. Wanafunzi wote wa shule ya malazi ya Kilindi lazima tuwachunguze. Sasa, uamuzi ni wako, fuata sheria au chukua mtoto wako urudi naye nyumbani. Chaguo ni lako.

8. **SEREFA:** Pato, mfungulie mwalimu sanduku… lakini kwani itamlazimu kuonyesha kila kitu alichobeba?

9. **SFX: SUITCASE BEING OPENED**

10. **MANENO:** Naam, ndivyo ilivyo. Lakini sawa: Safari hii wewe sitakuchunguza. Unaweza kufunga sanduku lako. Njozi zangu zinaniambia wewe si mtoto mtukutu.

11. **SFX: SUITCASE BEING CLOSED**

12. **PATO:** Shukrani Bw. Maneno.

13. **SEREFA:** Pato ni msichana mtiifu! Mbali na juhudi yake darasani, pia ni mkimbiaji hodari… tafadhali muhusishe ajiunge na timu wa wanariadha.

14. **PATO:** **(embarrassed)** Mama… lakini mimi si mzuri hivyo. Ninapenda kukimbia lakini sio kwenye mashindano.

15. **MANENO:** Shule yetu huongoza nchini katika mchezo wa riadha. Tunafurahia kupata nguvu mpya kwenye kikosi. Sawa, Pato – acha nikuonyeshe utalala wapi.

16. **SEREFA:** **(interrupts)** Emm... Bw. Maneno, kabla ya hayo, nina swali moja linalonikera... hebu nieleze, binti yangu kweli yu salama hapa? Kumaanisha wavulana wote hawa wanamzunguka. Nafahamu,

hii ni shule ya mseto, kweli nafaa kuwa na hofu?

17. **MANENO:** Mama, wewe ni mmoja kati ya wazazi wengi wanaouliza swali hilo. Lakini usihofu. Ndio, hii ni shule ya malazi kwa wavulana na wasichana, lakini kuna boma linalowatenganisha kila moja pande yao. Na yupo mlinzi kuhakikisha hakuna anayepenya kuingia asikostahili. Ni hakika kuwa bintio yu salama.

18. **SEREFA** Oh vyema.. hofu imenitoka.

19. **MANENO:** Pato, nifuate. Nitakupeleka kwenye bweni lako.

20. **PATO:** **(as she hugs and kisses her mum)** Kwaheri mama, nitakutumia barua hivi karibuni.

21. **SEREFA:** Kwaheri, mwanangu Pato. Nitakutembelea hivi punde. Utakuwa msichana mzuri, sivyo?

**MSIMULIZI:** Serefa anamuacha binti yake Pato chini ya utunzi wa Bw. Maneno, mkuu wa bweni. Lakini unaona ni wazo jema kuwaweka wavulana na wasichana katika shule moja ya malazi? Na unaweza kuwaamini waalimu? Kwa sasa, hata hivyo, tumuache Pato amakinike, ndiyo twende tukawaone Nuru na Jena. Wanawake hawa wawili ni marafiki tangu utoto wao. Wanaishi sehemu ya nchi inayoitwa Baruti ambayo hupendwa sana kuvamiwa na waasi. Jena ana katoto kachanga, na Nuru ana mimba ya miezi mitano. Wawili hao wametembea muda mrefu kutafuta kisima angalau

wapate tone la maji.

**SCENE TWO: NURU NA JENA KISIMANI**

| | | |
|---|---|---|
| **22.** | **SFX: FOREST AMB** | |
| **23.** | **SFX: SOUND OF WATER POURING INTO A BUCKET** | |
| **24.** | **NURU**: | Haya huyo Chambo wako anaendeleaje, Jena? Ana nafuu sasa? |
| **25.** | **JENA:** | Nuru, Chambo ana afya yake kama ndovu. Nimemuacha akimsumbuwa babake. Na wewe hali yako? Mtoto yu salama? |
| **26.** | **NURU:** | **(tired**) Nashukuru – uchovu tu kidogo. Ah Jena, natamani nizae hata sasa. Dulu anatamani sana kuitwa baba. Tena yuwataka kumzaa mamake… lakini nafikiri atakuwa mvulana. |
| **27.** | **JENA:** | Mbona mumeo atake msichana badala ya mvulana? |
| **28.** | **NURU:** | **(sarcastic)** Ndiyo… kwani kuna shida yoyote? |
| **29.** | **JENA:** | **(with emphasis)** Ati kuna shida? Bila shaka! Wanaume wa Kiafrika hupenda sana kuzaa watoto wa kiume. Huyo Dulu wako! Nafikiri uzungu umemtawala. |

**30.** **NURU:** La, nafikiri amegunduwa kuwa haijalishi kama mtoto ni msichana au mvulana – kitu muhimu ni kuwa atakuwa mtoto wetu. Hebu nimwagie maji tafadhali. Ndoo imejaa.

**31.** **SFX: WATER BEING POURED INTO A JERRY CAN**

**32.** **JENA:** Nuru… samahani leo sitakusubiri. Nina shangazi mngonjwa nampelekea maji. Anaishi kule maporomokoni, kwa hivyo hatutaandamana. Nisamehe sikukueleza mapema.

**33.** **NURU:** **(scared)** La! Tafadhali, Jena… usiniache peke yangu. Ni hatari!

**34.** **JENA:** We, usihofie! Hakuna lolote litakalokutokea. Uko salama. Nitakupitia nyumbani kwako kesho asubuhi, na tuje wote majini. Kwaheri, Nuru… na umpe salamu zangu mumeo Dulu.

(**Jena acts out carrying a heavy jerrycan of water on back**)

**35.** **NURU:** Sawa, nawe mpe risala zangu shangazi yako.

**36.** **SFX: JENA WALKING AWAY, singing under her breath**

**37.** **NURU**: **(whispers)** Itanibidi niharakishe... sipendelei kuwa hapa peke yangu saa hizi. Maficho ya waasi hayako mbali na hapa.

**38. SFX: WATER BEING HURRIEDLY POURED INTO CONTAINER**

**39. MSIMULIZI:** Nuru kweli katishika, lakini kwa sababu gani? Kweli ana haki ya kuhofu? Usibanduke. Lakini kwanza twende sehemu moja ya nchi ambapo kijana wa miaka kumi, Allan ameketi nje ya mgahawa, akipata kinywaji. Yuko na mamake, Precious, ambaye ndiye mzazi pekee. Precious amefuatana na mwanamume ambaye Allan hajawahi kumuona tena hapo awali. Huyu mgeni ni nani?

**40. <u>SCENE THREE: ALLAN AND HIS MOTHER IN CAFE WITH JOE</u>**

**41. SFX: CAFE ATMO**

**42. PRECIOUS:** Allan, kuna mtu nataka ukutane nae…

**43. SFX: DREGS OF SOFT DRINK BEING SLURPED THROUGH STRAW**

**44. PRECIOUS:** **(shouts)** Allan, wacha kufanya hivyo! Huyu mtoto! Hana adabu kabisa. Sasa nisikilize. Huyu ni mjombako, Joe. Hebu msalimie.

**45. ALLAN:** **(disinterested)** Hmm?

**46. PRECIOUS:** Msalimie anko Joe!

**47. ALLAN:** Shikamoo. – Kwani yule mjomba mwengine yuko wapi?

48. **PRECIOUS:** **(embarrassed)** Gani…?... Erm… Si … Sidhani …

49. **JOE:** Yule mjomba mwengine ameenda.

50. **ALLAN:** Yule ndiye nampenda kushinda anko wote.

51. **PRECIOUS:** **(at a loss for words)** Wee… Er… Allan, Nina hakika utampenda pia anko Joe.

52. **JOE:** Haya, Allan, mbona usiende ukanunue soda nyingine?

53. **SFX: COINS IN HAND**

54. **PRECIOUS:** Unasemaje ukipewa soda?

55. **ALLAN:** **(bored)** Asante.

56. **SFX: CHAIR MOVES, ALLAN LEAVES**

57. **PRECIOUS:** Joe, Pole kwa hayo. Natumai hujakasirishwa.

58. **JOE:** La, kamwe. Nafikiri ni kijana mkweli, akikuwa hivyo atakuwa mzuri. Lakini waonaje ukimweleza ukweli mapema? Mimi si mjombake. Mimi natazamia kuwa babake wa kambo.

59. **PRECIOUS:** La, la, Nafikiri ni vyema kusubiri… Tutamweleza baadae, atakapokuzoea. Asante kwa kunielewa. Natumai wawili nyinyi mutapata muda mzuri pamoja.

60. **JOE:** **(charmingly)** Oh, huna haja ya kuwa na wasiwasi kwa hilo, Precious. Watoto mimi hunipenda sana.

61. **MSIMULIZI:** Maneno ya Joe ni yale yale ambayo Precious amepanga kuyasikia masikioni mwake. Lakini unafikiri anafanya sawa kweli kumuamini Joe haraka hivi? Tutayang'amua hayo si punde… Lakini kwanza tumrudie Nuru, ambaye tayari kajaza maji pomoni ndooni mwake.

62. **<u>SCENE FOUR: NURU AT THE WATERHOLE</u>**

63. **NURU:** Sawa, ndoo imejaa. Haraka sasa – nahitaji kurudi nyumbani kabla…

64. **SFX: PICK-UP VAN APPROACHING ON ROUGH ROAD**

65. **NURU:** **(scared stiff)** Oh hapana! Tafadhali isiwe wao… wasiwe hao ni waasi!

66. **SFX: AUTOMATIC WEAPON - GUN SHOTS**

67. **SFX: NURU RUNNING**

**68. NURU:** **(spurring herself on)** Kimbia Nuru! kimbia!... La.. hapana.. wataniona… Na je wakinipiga risasi? Jifiche haraka!- nitajificha wapi - ??!

**69. SFX: NURU DIVES INTO WATERHOLE**

**70. NURU:** Tafadhali Mungu, usiwalete hapa kwenye maji. Nakuomba Mungu uwapitishe na kule kando...…

**71. SFX: PICK-UP VAN COMES TO A HALT. DOORS OPEN**

**72. (mean laughter from couple of men)**

**73. NURU:** Ah hapana…!

**HITIMISHO:**

Na kwa hayo tunamuacha Nuru, akijificha kisimani, tukihitimisha kipindi hiki cha **Noa bongo, jenga maisha yako**. Makala haya yanaitwa **"Wasaliti walo karibu"**, na hasa yanamulika maasi au dhulma za ngono barani Afrika. Kweli Nuru ataweza kuwaepuka waasi? Ni yapi yatakayompata Pato katika shule yake hiyo mpya? Na anko Joe ataelewana vipi na Allan? Kwa haya na mengine usikose kipindi kijacho. Kama utahitaji kusikiliza kipindi hiki tena, au kututumia ujumbe au maoni, tembelea tovuti zetu dw.de/lbe au mtandao wetu wa Facebook. Mpaka makutano yetu tena. Alamsiki.